# HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

## MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA KWANZA 2023/2024 ULIOFANYIKA TAREHE 17.11.2023 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

***Mahudhurio:***

***Wahe. Madiwani:***

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Gerald Samwal Ng'ong'a | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Ezra Masana Bugingo | Diwani |
| 3. | Mhe. Ernest Marwa Sama | Diwani |
| 4. | Mhe. Deo Alfred Magori | Diwani |
| 5. | Mhe. Albet Machiwa | Diwani |
| 6. | Mhe. Geofrey Samwel Juma | Diwani |
| 7. | Mhe. Charles Chacha Nyambaki | Diwani |
| 8. | Mhe. Juma Gradus Thondoe | Diwani |
| 9. | Mhe. Andericus Okwach Sariro | Diwani |
| 10. | Mhe. Joseph Ogaja Mbega | Diwani |
| 11. | Mhe. Samson Kagutu | Diwani |
| 12. | Mhe. Paulo Martine Amuko | Diwani |
| 13. | Mhe. Adriano Johanes Nyawambo | Diwani |
| 14. | Mhe. Zuberi Mohamed Kinanda | Diwani |
| 15. | Mhe. Sylvana Ndemera | Diwani |
| 16. | Mhe. Khalphan Abdul Bimbireh | Diwani |
| 17. | Mhe. Julitha Athony Maige | Diwani |
| 18. | Mhe. Vivian Kyage Nyamabwa | Diwani |
| 19. | Mhe. Fideria Otonya Rangi | Diwani |
| 20. | Mhe. Nelson Ores Simba | Diwani |
| 21. | Mhe. Shelta John Mang'era | Diwani |
| 22. | Mhe. Angelus Mwita Wambura | Diwani |
| 23. | Mhe. William Nestory Marwa | Diwani |
| 24. | Mhe. Justine Rugoye Nyoswede | Diwani |
| 25. | Mhe. Ayoi Musa Sonde | Diwani |
| 26. | Mhe. Felister Awil Nyakwaka | Diwani |
| 27. | Mhe. Hellen Ezekiel Magige | Diwani |
| 28. | Mhe. Laurent Abich Adriano | Diwani |
| 29. | Mhe. Jumanne Ally Oketho | Diwani |
| 30. | Mhe. Roja Lazaro Akuku | Diwani |
| 31. | Mhe. Zablon Segere Mwita | Diwani |
| 32. | Mhe. Opino Beya Nickson | Diwani |
| 33. | Mhe. Edina Charles Oloo | Diwani |
| 34. | Mhe. Godfrey Dalmas Nyagwa | Diwani |

***Wasiohudhuria kwa taarifa:***

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Jaffari W. Chege | Mbunge |

***Mahudhurio:***

***Watendaji:***

| | |
|---|---|
| 1. Adv. Abdul O. Mtaka | Mkurugenzi Mtendaji–Katibu |
| 2. Bw. Mbujilo G.M | Afisa Utumishi (W) |
| 3. Bw. Paul M. Amos | Kny: Katibu Tume ya Walimu (TSC) |
| 4. Bw. Patrick Mathias | Kaimu Mdhibiti Mkuu Ubora wa Shule |
| 5. Bw. Frances Mahimbo | Afisa Usafi na Mazingira (W) |
| 6. Bw. Comedius Mwananzila | Afisa Tarafa |
| 7. Bw. Kessy Omary Hamisi | Afisa Tarafa |
| 8. Bw. Alex Ifunya | Mwanasheria wa Halmamshauri |
| 9. Bw. Cosmas Mwantisya | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 10. Bw. James C. Chitumbi | Afisa Kilimo Mifugo na Uvuvi |
| 11. Bw. Jairo Omeme | Kaimu Afisa TEHAMA |
| 12. Bw. Bartholomew B. Matoke | Kaimu Afisa Manunuzi |
| 13. Bw. Abdallah S. Mikui | Afisa Utamaduni |
| 14. Bw. Emmanuel Shayo | Kny: Mganga Mkuu |
| 15. Bw. Maro Makuru | Kaimu Mweka Hazina |
| 16. Bw. Mtuli Jumanne | Mratibu wa TASAF |
| 17. Bw. Joseph T. Nyamwanda | Afisa Tarafa |
| 18. Bw. Emmanuel Zakaria | Afisa Tarafa |
| 19. Bw. Claud Katura | Kny: Afisa Usafirishaji |
| 20. Bw. Salim Agwanda | Kaimu Afisa Biashara |
| 21. Bw. Pauline Mathias | Kaimu Afisa Elimu Awali na Msingi |
| 22. Eg. Ramadhani Mcharo | Mhandisi wa Ujenzi |
| 23. Bw. Iman R. Mgonja | Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 24. Bw. Folkward Mchami | Afisa Elimu Sekondaria (W) |

***Wageni waalikwa:***

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Juma I. Chikoka | Mkuu wa Wilaya |
| 2. Bw. Boniphace Chambi | Katibu Tawala (W) |
| 3. Bi. Agnes Kimea | Kny: Katibu Tawala (M) |
| 4. SSP. Festo G. Ukulule | OCD – Rorya |
| 5. Spewadi S. Haule | OCD – Kinesi |
| 6. Bw. Saidi Gingo | OCD – Shirati |
| 7. Bw. Petro Chacha Mang'era | Kaimu Meneja RUWASA |
| 8. Bi. Baturi Mshana | Kny: Afisa Usalama |
| 9. Bw. Eliwako Kitua | Kny: Kamanda TAKUKURU |
| 10. Eng. Hussein Abbas | Meneja RUWASA |
| 11. Bw. Zebedayo A. Gadau | Meneja TANESCO |

***Waandishi wa Habari***

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Frankius Cleophace | RFA / STAR TV |
| 2. | Bw. Thomas Nkaina | Habari Rorya |
| 3. | Bw. Jumanne Ntono | TBC |

***Sekretarieti:***

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Rahan M. Amosy | Mwandishi wa Vikao vya Halmashauri |
| 2. | Bw. Marline M. Matara | Mwandishi wa Vikao vya Halmashauri |
| 3. | Bi. Florah M. Breck | Katibu Mahsusi |
| 4. | Bw. William Kibasso | Mratibu wa Vikao |
| 5. | Bi. Devotha Masiaga | Msaidizi wa Ofisi |
| 6. | Bw. Paul Maloda | Cashier |

***Agenda:***

1. Kufungua Mkutano.
2. Utambulisho wa wageni.
3. Kusoma na kuridhia agenda.
4. Maswali ya papo kwa papo kwa Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi Mtendaji (w).
5. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Nne 2022/2023 uliofanyika tarehe **30.08.2023**
6. Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Nne 2022/20233 uliofanyika tarehe **30.08.2023**
7. Muhtasari wa taarifa za Kamati za Kudumu kwa Robo ya Kwanza 2023/2024
8. Kuwasilisha na kujadili taarifa za utekelezaji wa Taasisi (RUWAS, TARURA NA TANECO)
9. Kufunga Mkutano.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.01/11/2023: KUFUNGUA MKUTANO**

Mwenyekiti alisimama na kuwasalimia wajumbe wote waliokuwa wamehudhuria kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani kwa kipindi cha Robo ya Kwanza 2023/2024 na kuwakaribisha wajumbe waliohudhuria kwenye Mkutano huo na kuwaeleza wajumbe kuwa Mkutano huo ni wa kawaida hivyo wanatakiwa kutoa michango yao ya mawazo kwa maslahi mapana ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.02/11/2023: UTAMBULISHO WA WAGENI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya alimkaribisha Mwenyekiti wa Halmashauri ili aweze kuwakaribisha na kuwatambulisha wageni mbalimbali waliohudhuria kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Kwanza kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.03/11/2023: KUSOMA NA KURIDHIA AGENDA**

Jumla ya agenda Tisa (09) zilizokuwa zimepangwa zilisomwa na kupokelewa na wajumbe. Aidha, wajumbe walizidhibitisha agenda hizo ili ziweze kujadiliwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Kwanza 2023/2024.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.04/11/2023: MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MHE. MWENYEKITI WA HALMASHAURI NA MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

Wajumbe waliojiorodhesha mapema kwa mujibu wa Kanuni walipewa fursa ya kuuliza maswali ya papo kwa papo. Aidha, wajumbe hao walipewa majibu na ufafanuzi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) na Mwenyekiti wa Halmashauri na wote waliridhika.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.05/11/2023: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA NNE 2022/2023 ULIOFANYIKA TAREHE 30.08.2023**

Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Nne 2022/2023 uliofanyika tarehe **30.08.2023,** ulisomwa na kupokelewa na wajumbe. Aidha, wajumbe waliupitia muhtasari huo ukurasa kwa ukurasa hadi mwisho. Hatimaye waliuthibitisha ili kumbukumbu halali ya vikao vya Baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.06/11/2023: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA NNE 2022/20233 ULIOFANYIKA TAREHE 30.08.2023**

***Kipengele kilichohusu Afisa Usafi na Mazingira kuandikiwa barua ya Onyo***

***Azimio:***

Iliazimiwa kwamba, Afisa Usafi na Mazingira aandikiwe barua ya **ONYO** kwa kudanganya Baraza la Madiwani na Mkurugenzi Mtendaji (W) ya kumtaka kutoa maelezo ya kina kuhusu Dampo lililopo shule ya Sekondari Ngasaro.

***Utekelezaji:***

Baada ya Baraza kutoa maagizo kuwa Afisa Usafi na Mazingira aandikiwe barua ya onyo, Mwenyekiti wa Halmashauri alipata nafasi ya kufanya kikao na WDC ya kata ya Mkoma na kubaini kuwa maelekezo yaliyotolewa awali ya kuhamishwa kwa dampo yalikuwa sahihi na kupelekea kufutwa kwa azimio lililoazimiwa. Aidha wajumbe walishauri kuwa hata kama taka zitakuwa zimesogezwa lakini eneo bado sio rafiki kwa afya ya wakazi na wanafunzi wanaosoma katika shule ya sekondari Ngasaro. Baada ya ushauri huo wajumbe waliagiza kama ifuatavyo; -

***Azimio:***

Iliazimiwa kwamba kamati ya maendeleo ya kata ya mkoma watafute eneo la kuhamishia dampo kwa ajili ya usalama wa wakazi.

***Kipengele kilichohusu Kaimu Afisa Manunuzi***

***Azimio:***

Iliazimiwa kwamba; Kaimu Afisa Manunuzi Ndugu Dominian Mpombe asimamishwe majukumu yake ili kupisha uchunguzi.

***Utekelezaji:***

Azimio limezingatiwa na tayari Ndg. Dominia Mpombe ameshaandikiwa barua yenye Kumb. Na. HWR/CF/02/2/48 ya tarehe 04.09.2023 ili aweze kupisha uchunguzi.

***Kipengele kilichohusu Hoja za Ukaguzi***

***Azimio:***

Iliazimiwa kwamba; Wakuu wa Idara na Vitengo waandikiwe barua na Mkurugenzi Mtendaji (W) ya kuwataka kutoa majibu kwenye Hoja za Mkaguzi, ndani ya siku 14 kuanzia tarehe **30.08.2023.**

***Utekelezaji:***

Azimio limezingatiwa na tayari Wakuu wa Idara na Vitengo wamekwisha andikiwa barua yenye Kumb.Na.HWR. C.06/12/88 ya tarehe 04.09.2023 ya kuwataka kutoa majibu ya Hoja za Mkaguzi wa Ndani.baada ya kupokea utekelezaji wajumbe waliagiza/kutoa maelekezo kama ifuatavyo; -

***Azimio:***

Iliazimiwa kwamba kikao kijacho cha Mkutano wa Bazara la Madiwani iwasilishwe taarifa ya majibu ya Hoja za ukaguzi ambazo zilikuwa hazijajibiwa.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.07/11/2023: MUHTASARI WA TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU KWA ROBO YA KWANZA 2023/2024**

Wenyeviti wa Kamati za Kudumu (Kamati ya Elimu, Afya na Maji, Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira, Kamati ya Maadili, Kamati ya Kuthibiti UKIMWI na Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa kamati zao kwa kipindi cha Robo ya Kwanza 2023/2024 na taarifa hizo zilipokelewa na wajumbe na kisha kutoa ushauri na maelekezo kama ifuatavyo: -

**Katika kipengele kilichohusu Ujenzi wa miradi na miundombinu mbalimbali inayotekelezwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya:**

Wajumbe walishauri Halmashauri ione namna ya kuboresha stendi ya Ingri chini ili kusaidia shughuli kuendelea na nyumba zisiwe magofu. Aidha walishauri tuboreshe miundombinu ya mwalo mikubwa tuliyonayo ili kusaidia uchukuzi wa samaki na dagaa/ufanyikaji mzuri wa biashara. Pia wajumbe walishauri tuisaidie shule ya msingi Kinesi A upande wa miundombinu kwa kuwa ni kongwe na chakavu. Halmashauri isaidie ukamilishaji wa Zahanati ya Kyanyamsana ili kusaidia wananchi kwa kuwapunguzia mwendo mrefu kufata huduma kituo cha afya Kinesi. Halmashauri ione namna ya kuisaidia shule ya sekondari Kinyenche kupata Hosteli ya wanafunzi na miundo mbinu ya umeme.

**Katika kipengele kilichohusu mikopo ya Vijana, Wanawake na Watu wenye ulemavu:**

Wajumbe walishauri Idara ya Maendeleo ya Jamii watusaidie kuwasiliana na mamlaka ya Mikopo ili kujua muhafaka wa utoaji wa mikopo ya Vijana, Wanawake na Watu wenye ulemavu kwa kuwa fedha zipo na tunahitaji ziende kwa walengwa. Aidha wajumbe walishuri kufatilia marejesho ya mikopo ambayo Halmashuri ilishakopesha kwa vikundi ili kupata fedha hizo kwa ajili ya vikundi vingine kukopeshwa.

**Katika kipengele kilichohusu Afya na Mazingira:**

Wajumbe walishauri Halmashauri ione namna ya kuongeza wahudumu katika Zahanati tulizonazo ili kuweza kumudu kutoa huduma kusudiwa kwa wananchi bila malalamiko. Aidha wajumbe walishauri tuone namna sahihi ya kuajiri walinzi katika vituo vyetu vya kutolea huduma za Afya ili kupunguza adha ya wizi wa vifaa tiba. Pia wajumbe walishauri tuone namna ya kusimamia suala la usafi katika maeneo/ senta zetu kubwa kama Shirati, Utegi, Nyanchabakenye na Kinesi ili kuepusha mrundikano wa taka na kuweka mazingira salama kwa ajili ya wakazi wa maeneo hayo.

**KUMB.MUHT.BRZ.NA.08/11/2023: KUWASILISHA NA KUJADILI TAARIFA ZA TAASISI ZA RUWASA, TARURA NA TANESCO**

Wakuu wa Taasisi (RUWASA, TARURA na TANESCO) waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa kamati zao kwa kipindi cha Robo ya Kwanza 2023/2024 na taarifa hizo zilipokelewa na wajumbe na kisha kutoa ushauri na maelekezo kama ifuatavyo:

**Katika kipengele kilichohusu taarifa ya RUWASA:**

Wajumbe walipongeza juhudi na shughuli zinazotekelezwa na taasisi katika maeneo mbali mbali ya Halmshauri na walishauri katika Miradi inayotekelezwa na taasisi basi wakamilishe kwa wakati ili kuepusha usumbufu/adha kwa wananchi kwa kuwa miradi mingi mitaro ya mabomba haifukiwa kwa wakati na kuleta madhara. Aidha wajumbe walishauri taasisi kuboresha miundombinu yao ili kusaidia wananchi kupata maji safi na salama kama kata ya Nyaburongo kuna shida ya kupata maji safi na salama.

**Katika kipengele kilichohusu taarifa ya TARURA:**

Wajumbe walipongeza juhudi na shughuli zinazotekelezwa na taasisi katika maeneo mbali mbali ya Halmshauri kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa kuboresha miundo mbinu ya barabara na walishauri taasisi kuona namna ya kuboresha barabara za vitongoji/mitaa katika maeneo yote yanayopatikana katika Halmashauri pamoja na eneo la makao makuu ya Halmashauri kwa kuwa barabara za mitaa hazipo na zilizopo sio Rafiki kwa matumizi kama barabara ya saro.

**Katika kipengele kilichohusu taarifa ya TANESCO:**
Wajumbe walishauri kuwa Meneja wa TANESCO kuweka uwiano sawa wa ugawaji/usambazaji wa umeme katika vijiji na vitongoji kwa kuwa umeme mara nyingi unafika kwenye senta lakini kwenye vitongoji haufiki na kwenye vitongoji ndipo wananchi wengi walipo. Wajumbe pia walishauri taasisi ione namna ya kuboresha miundombinu ya umeme ili kupunguza adha ya kukatika kwa umeme mara kwa mara.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.09/11/2023: KUFUNGA MKUTANO**
Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote waliohudhuria kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Kwanza 2023/2024. Aidha aliwaomba wajumbe kushirikiana kwa pamoja (Waheshimiwa madiwani na wataalamu) kusimamia vyanzo vya mapato na mazingira kwa ajili ya kuisaidia Halmashauri kupata mapato ya kutoka ili kuweza kujiendesha. Hatimaye alitamka kufunga mkutano majira ya saa 10:40 Jioni huku akiwatakia wajumbe wote safari njema.

**Muhtasari huu umethibitishwa na kusainiwa tarehe** 08/02/2024

**Sahihi**............................................ **Sahihi**............................................

**Jina** ABDUL MTAKO **Jina** GERALD NGONGA
**KATIBU** **MWENYEKITI**